

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI NGERENGERE
S.L.P 23, NGERENGERE – MWAKA 2021**

NAMBA YA SIMU; 0787 10 64 14/ 0715 10 64 14.

Kumb: Na NDSS/FKKS/01/2021.

JINA

ANUANI YA MZAZI/MLEZI.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGERENGERE DAY WILAYA
YA MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021.**

1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya sekondari Ngerengere Day ipo umbali wa **km 1** toka kituo cha mabasi ya Ngerengere mjini. Shule ipo katika kijiji cha Ngerengere, kata ya Ngerengere, Tarafa ya Ngerengere, Halmashauri ya wilaya ya Morogoro, Mkoa wa Morogoro.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **28/01/2021**.

2.0 MABO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE.

- a) Suruali mbili rangi ya **DAMU YA MZEE ESTIM NO 1** kwa wavulana na shati nyeupe mikono mifupi, na sketi mbili rangi ya **DAMU YA MZEE STIM NO 1** kwa wasichana na blauzi rangi nyeupe mikono mifupi.
 - Mshono; suruali ziwe na marinda 2; mifuko mitatu (mifuko ya mbele isiwe ya kuchimba wala kubandika kama jinsi, isiwe ya kubana chini (modo) kwa wasichana rinda boksi iwe ndefu kupita magoti (inchi sita toka gotini kushuka chini isipungue inchi sita toka magotini kwenda chini)
- b) Wanafunzi wote wanatakiwa kuweka alama ya **1** kwenye shati mabega yote ili kuonyesha kidato cha kwanza (alama hiyo ni kipande cha kitambaa cha suruali au sketi yake).
- c) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule (sketi mbili rangi ya **DAMU YA MZEE ESTIM NO 1**) ziwe ndefu kufunika miguu kufikia vifundo vya miguu, blauzi au nusu kanzu kufikia magoti, mikono mirefu, juba rangi nyeupe mbili ziwe ndefu kufunika mikono kwenda chini. **MSHONO WA SKETI NI RINDA BOX.**
- d) Sare za michezo kwa shule hii ni rangi ya bluu na rangi ya njano na Tshirt zifanane rangi na bukta, kwa wasichana ni bukta mbili ziwe ndefu kupita magoti rangi ya bluu na njano Tshirt rangi zifanane na bukta.
 - Wote wawe na tracksuit rangi ya blue au njano.
- e) Viatu vya ngozi pea mbili vya kufunga na Kamba rangi nyeusi na visiwe na kisigino kirefu wala visiwe buti, wasichana watavaa soksi nyeupe zisizo na alama na wavulana watavaa soksi nyeusi zisizo na alama yeyote.

2.2 Daftari 11 kubwa (counter books) kalamu na mkebe wa hesabu mmoja oxford.

3.0 Wavulana fyekeo moja.

3.1 Wasichana ndoo ndogo ya lita 10 kwa ajili ya usafi shuleni.

3.2 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebiswa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambyo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa uongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhuria mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa umakini kwa maandalio ya jioni (preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kiukamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Kutokutumia lugha za matusi katika maeneo yote ya shule na nje ya shule.

3.4 MAKOSA YAFUATAYO YATAPELEKEA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- a) Wizi.
- b) Uasherati (uzinzi) na ushoga.
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile; uvutaji bangi, cocaine, ulaji mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana na kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/ kupata kimba
- i) Kuo au kuolewa
- j) Kutoa kimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mikononi.

3.5 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- a) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- b) Fomu ya mzazi ya kukiri kukubalina na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

3.6 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

" KARIBUNI SANA NGERENGERE SEKONDARI "

.....
PETRO H. TUMAI

MKUU WA SHULE.

HEADMASTER
NGERENGERE DAY SEC. SCHOOL
P. O. Box 23, NGERENGERE